Barua ya wazi kwa watu walio bakwa au kuuzwa utumwani:

Kitu kibaya sana kimekutokea, kitu ambacho hakipaswi kumtokea mtu yeyote kamwe. Baadhi ya watu hupatwa na kiwewe kama chako wakijua kwamba sio kosa lao. Bahati mbaya, wengineo wengi uona aibu na kujichukia, na baadhi huwa na fikira potovu kwamba mateso yao ni adhabu kutoka kwa Mungu. Ndio maana tunataka kujibu baadhi ya maswali yafuatayo muhimu .

Basi kwa nini watu hujilaumu?

Njia moja wapo ambayo watu wanajaribu kudhibiti hali mbaya sana. Kwa mfano, wanaweza kufikiria kwamba kama ni wema sana au wakiomba sana msamaha, hamna chochote kibaya kitakacho watokea tena. Lakini sio sawa kujilaumu. Pia, unyonya nguvu unayohitaji kutatua namna utakavyo fanya ili uweze kustahimili mateso yako.

Je inakuwaje kama nilifanya kitu cha kijinga au kibaya ambacho kilisababisha ubakaji au kuuzwa utumwani?

Bila kujali ulichofanya, mtu anaekubaka au kukuuza utumwani au kukunyima uhuru wako hana utetezi wowote. Mtu aliyekuumiza alifanya kosa la jina na ufungwa jela katika nchi nyingi kwa kufanya tendo hili. Wewe ni mwathiriwa wa tendo la jinai. Kama utakasirika, kasirikia hali hiyo au mhalifu, na sio ujikasirikie mwenyewe. Watu wakulaumu PEKEE ni wale waliosababisha uteseke.

Je, inakuwaje kama familia na marafiki zangu wananilaumu mimi?

Hicho ni moja wapo ya vitu vyenye kutia huzuni sana: wakati familia na marafiki wanapo mlaumu mwathiriwa badala ya mtu anaebaka au kunyima watu uhuru wao. Kama wakisoma haya maadiko, wanaweza kuanza kuelewa kwamba SIO kosa lako. Lakini hata kama familia na marafiki hawaachi kukulaumu, lazima wewe uache kujilaumu mwenyewe ili uweze kuanza kupona.

Je kitu hiki kimetokea kwa sababu Mungu alikuwa ananiadhibu?

Hapana! Wengi wetu tunakuwa tukiwa na fikira kwamba Mungu mwenye nguvu zote na wakujua vyote, atatuzawadia kama tukiwa wema na kutuadhibu kama tukiwa waovu. Kwa hivyo, kama kitu kibaya kikitokea, wengi wetu tunasadiki kwamba tumeadhibiwa na Mungu. Lakini bila shaka unafahamu watu wabaya ambao hawaadhibiwi dhambi zao na watu wema ambao wamepata magonjwa mabaya au wamekumbwa na majanga. Kwa hiyo unajua kwamba Mungu hatoi hukumu yake katika maisha haya kila wakati. Licha ya hayo, hamna kitu chochote ambacho kinaweza kuhalalisha kubakwa

au kuuzwa utumwani, kwa sababu hamna mtu anaestahili hicho.

Kwa nini Mungu anaruhusu watu wabakwe au wauzwe utumwani?

Mungu aliumba dunia ambayo watu wana uamuzi huru, na kuna baadhi ya watu wanachagua kuwa waovu – kubaka au kuuza watu utumwani. ***Niliuzwa utumwani kulipia deni lililosababishwa na "tendo la Mungu". Je, sio Mungu aliyesababisha hilo?***

Mungu aliumba dunia inayoongozwa na utaratibu wa jambo la asili, ina maana kwamba kuna "majanga ya kiasili" kama mafuriko au ukame, ambavyo vinasababisha umaskini na madeni. Lakini Mungu hasababishi majanga au umaskini ili kuadhibu watu.

Je, lakini Biblia haiongelei kuhusu Mungu kuadhibu watu kwa mafuriko na ukame?

Ndio ila Biblia iliandikwa kabla wana sayansi hawajajifunza juu ya utaratibu wa jambo la asili. Kwa mfano, wakati mafuriko yanapotokea, watu wema pamoja na waovu uteseka wote. Kwa nini Mungu aadhibu watu wasio na makosa wengi vile kusudi afundishe waovu wachache ubaya wa matendo yao?

Na Je, Biblia haizungumzii juu ya kulinda wale ambao "utembea katika kivuli cha mauti?"

Kama ulisali ukiomba kulindwa na hakikutokea, haina maana kwamba Mungu hakukujali au amekuadhibu.

Katika hali za hatari, kwa mfano kama vita, raia na askari wengi wema na waovu uumia sawa Mungu yuko nasi wakati tunapokuwa katika sehemu za kutisha na utupa nguvu.

Ninaweza kufanya nini nijisikie nafuu?

- Anza kwa kujisamehe. Umeshaumizwa vya kutosha: usiendelee kujiumiza mwenyewe.
- Jaribu kutofanya hasira zako na maumivu yako yakufanye uwe na kisirani au ukose matumaini. Tumia njia zilizo nzuri kuondoa hasira kama vile kupiga mto au wakati ukiwa peke yako, kupiga uyole wa kujiondolea hisia ya kutokuwa na

uwezo. Au tumia hasira kama nguvu ya kiakili ya kushinda hali yako.

- Waathiriwa wengi usaidiwa kwa kukutana na watu wengine ambao wamepitia hali kama yao. Uwa wanaunda kundi la kuegemeana ili kusaidiana kupata nguvu na uwezo wa kuendelea.

- Jaribu kukusanya nguvu ya kujenga upya maisha yako na kusaidia wengine kufanya hivyo pia.

- Jiambie ukewli: kwamba unapendwa na Mwenyezi Mungu bila kujali kitu chochote kilichokutokea.

- Omba uondolewe maumivu, aibu na kujihisi kwamba wewe ndio wa kulaumu. Omba uwe na nguvu, nia na utashi vya kukuwezesha kustahimili yaliyo kutokea na kuweza kujenga maisha ya mbeleni yaliyo na nafuu. Mruhusu mungu akusaidie kuvuka haya yote.

Watu wengi ulimwenguni wanajaribu kuzuia jinai za ubakaji na uuzaji wa watu utumwani, pia wanakuombea wewe pamoja na wengine walioteseka. Wako kama sisi, wanakuona wewe kama shujaa aliyesalimika na bila lawama kabisa. Tumekuandikia barua hii na kukutumia pamoja na sala za upendo kwa kupona kwako,

Dada zako walioAnglican Women's Empowerment
(Uwezesho wa Wanawake wa Kianglikana)

Wasiliana na Anglican Women's Empowerment juu ya baruia hii, andika barua pepe kwa awetoday@gmail.com. Kutoa nakala zaidi za barua hii, nenda www.anglicanwomensempowerment.org.